**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA AFYA (FUNGU 52) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025]*

Idara ya Kamati za Bunge
Ofisi ya Bunge,
Mtaa za Makole
S.L.P. 941
**41104 DODOMA**

**11 Mei, 2026**

## YALIYOMO


YALIYOMO ........................................ i
SEHEMU YA KWANZA ........................................ 1
1.0 UTANGULIZI ........................................ 1
1.1 Maelezo ya Jumla ........................................ 1
1.2 Muundo wa Taarifa ........................................ 1
1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ........................................ 2
1.3.1 Msingi wa Taarifa ........................................ 2
1.3.2 Mbinu Zilizotumika ........................................ 2
1.3.3 Wigo na Mipaka ya Taarifa ........................................ 3
SEHEMU YA PILI ........................................ 5
2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ........................................ 5
2.1 Maelezo ya Jumla ........................................ 5
2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ........................................ 6
2.2.1 Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo ........................................ 7
2.2.2 Utekelezaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati Mwaka 2025/2026 ........................................ 10
2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ........................................ 11
2.2.4 Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2025/2026 14
2.3 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ........................................ 18
2.3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027 ........................................ 19
2.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ........................................ 21
2.4 Masuala Mengine Muhimu kuhusu Mpango wa Wizara kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 ........................................ 23
2.4.1 Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ........................................ 23
2.4.2 Uwekezaji wa Viwanda vya Kuzalisha Bidhaa za Dawa ........................................ 25
SEHEMU YA TATU ........................................ 26
3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ........................................ 26
3.1 Maoni ........................................ 26
3.2 Ushauri wa Kamati ........................................ 26

3.3 HITIMISHO .......................................................................................... 30
3.4 SHUKRANI ............................................................................................ 30

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inabainisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa taarifa na kuonesha taarifa inavyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa. Kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehumu kuu tatu ambazo ni:

(a) Sehemu ya Kwanza inayotoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati katika kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii;

(b) Sehemu ya Pili inayobainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(c) Sehemu ya Tatu inayobainisha Maoni, Ushauri, Hitimisho na Shukrani.

## 1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi

### 1.3.1 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kuchambua bajeti unatokana na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ambacho kimeainisha moja ya majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ni kushughulikia Bajeti ya Wizara inayoisimamia. Aidha, Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka unaoisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka unaofuata kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (5) ya Kanuni za Bunge. Baada ya hatua hiyo, nawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

### 1.3.2 Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inabainisha mbinu zilizotumika kufanyia kazi hoja hii kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 (a) (iii) ya Kanuni za Bunge. Lengo ni kujenga msingi wa kuwa rejea madhubuti, inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali za uchambuzi zikiwemo kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa mawasilisho ya Wizara na majibu kwa hoja mbalimbali ulifanyika kwa njia ya ulinganisho kimaudhui na uhalisia. Matokeo ya kufanya hivyo, ni kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi.

### 1.3.3 Wigo na Mipaka ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia madhumuni ya Taarifa hii Bungeni, maudhui yake yanagusa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ufafanuzi unaotolewa unahusu uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati Bunge linapitisha bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha. Eneo lingine ni makadirio ya maduhuli kwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ulinganisho wa bajeti na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Mambo hayo kwa ujumla wake, yanahusika katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi. Kamati hii ambayo ni tegemeo la Bunge katika kuisimamia, kuifuatilia na kuishauri Serikali kuhusu Afya, ilifanyia kazi maeneo hayo. Mazingatio makubwa yaliwekwa kwenye lengo Kuu la Serikali lililoelezwa

kwenye Ibara ya 8 (1 (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, ambalo, ni ustawi wa wananchi.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu Muundo wa Taarifa za Kamati, sehemu hii inaeleza kwa kina mambo yote yaliyochambuliwa na Kamati. Maelezo yanayotolewa yamegawanyika katika maeneo makuu mawili makuu ambayo ni:

(a) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, unaolenga kutathmini kiwango cha utekelezaji wa mapato na matumizi, kubaini changamoto zilizojitokeza pamoja na kushauri hatua stahiki; na

(b) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, unaolenga kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi kwa kuzingatia uhalisia wa mapato, vipaumbele vya kitaifa na ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma.

**Mheshimiwa Spika**, Mpangilio huu unalisaidia Bunge kupata mtazamo jumuishi wa mwenendo wa utekelezaji wa bajeti iliyopita na mwelekeo wa bajeti inayopendekezwa, na hivyo kuimarisha uwajibikaji, uwazi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kabla ya kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Lengo la kufanya hivyo, ni kupata taswira halisi ya mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali, kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza, pamoja na kupima kiwango cha ufanisi katika utekelezaji wa mipango iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huu umeiwezesha Kamati kupata uzoefu wa mwaka uliopita, kubaini maeneo yanayohitaji kuongezewa nguvu na kujenga msingi madhubuti wa ushauri unaotolewa kwenye Taarifa hii. Aidha, uchambuzi uliofanyika, unaliwezesha Bunge kutoa ushauri wa kibajeti na kuimarisha uwajibikaji wa Serikali katika matumizi ya rasilimali za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilichambua mambo matano (5) mahususi ambayo ni:

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Ukusanyaji wa Maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge;

(iii) Utekelezji wa Miradi ya Maendeleo;

(iv) Utekelezaji wa kazi zilizokuwa zimepangwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(v) Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2026.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa mambo hayo umewezesha tathmini jumuishi ya ufanisi wa utekelezaji wa bajeti. Aidha, maeneo hayo ni muhimu katika kuonesha mwenendo wa mapato, matumizi na utekelezaji wa mipango ya Serikali. Hali hiyo inasaidia kubaini mafanikio, changamoto na kutoa ushauri wenye tija. Kwa ujumla uchambuzi huu, unaliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi, uwazi na kwa kuzingatia malengo yaliyokusudiwa.

### 2.2.1 Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilitembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Afya. Jumla ya miradi sita (6) ilitembelewa na kukaguliwa katika mkoa wa Dar es Salaam. Miradi hiyo ni ifuatayo: -

(a) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana (Mradi Namba 5411);

(b) Uimarishaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (Mradi Namba 5412);

(c) Ujenzi na Ununuzi wa Vifaa Tiba vya Upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (Mradi Namba 5419);

(d) Ukarabati wa Jengo la Wagonjwa wa Nje *(Out-Patient Department)* katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo

(*Muhimbili Orthopaedic Institute-MOI*) (Mradi Namba 5491);

(e) Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (Mradi Namba 5487);

(f) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Temeke (Mradi Namba 5411); na

(g) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mwananyamala (Mradi Namba 5411).

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo, imeiwezesha Kamati kujiridhisha na hali halisi ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa, kiwango cha matumizi ya fedha za umma, pamoja na maendeleo yaliyofikiwa katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi. Kupitia ufuatiliaji huu, Kamati imebaini mafanikio yaliyopatikana, changamoto zinazoathiri utekelezaji wa miradi, na maeneo yanayohitaji uboreshaji wa haraka.

**Mheshimiwa Spika**, Katika miradi iliyokaguliwa, ipo miradi ambayo haijakamilika lakini utekelezaji wake umeanza na miradi ambayo utekelezaji wake haujaanza. Hali hiyo inatokana na kuwepo kwa changamoto mbalimbali kama vile kutokutolewa kabisa kwa fedha au kucheleweshwa kutolewa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Moja ya miradi mikubwa na ya kimkakati kwa Taifa ambao hauaanza kutekelezwa ni mradi namba 5487 unaohusu Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili *(New Muhimbili)*. Mradi huu utakamilika, utasaidia nchi kuimarika kwa kiwango kikubwa katika utoaji wa huduma za afya za ubingwa

wa juu na kuiweka Hospitali ya Taifa Muhimbili katika nafasi ya juu kama kituo bora cha mafunzo ndani ya Ukanda wa Afrika Mashariki. Aidha, Hospitali ya Taifa Muhimbili itakua kwenye nafasi bora ya kupata ithibati ya Kimataifa, itakayosaidia kutambulika Kimataifa na kuimarisha Tiba Utalii nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huo wa Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili unatarajia kuanza kutekelezwa mara baada ya kukamilika kwa taratibu za michoro na usanifu wa jengo.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa mradi mwingine ambao ulitembelewa na kuonekana uwezekano wa kutokamilika kwa wakati ni mradi namba 5491 unaohusu Ujenzi wa Jengo la Kuhudumia Wagonjwa wa Nje katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI). Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Septemba, 2024 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2026 ambapo hadi Kamati ilipotembelea mradi mwezi Machi, 2026 ni asilimia 34 ya fedha imetolewa.

**Yatokanayo na Ziara za Ukaguzi wa Miradi**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo, yamebainika mambo yafuatayo: -

(a) Uwekezaji mkubwa wa Mitambo, Mashine na Vifaa Tiba katika hospitali zote zilizokaguliwa;

(b) Fedha za miradi kutokutolewa au kutolewa kwa kuchelewa licha ya mwaka wa fedha kuelekea ukingoni;

(c) Upungufu wa Wataalam wa Afya, Mfano; Wataalamu wa Tiba Mionzi na Madaktari Bingwa na Bingwa Bobezi

(d) Uwepo wa idadi kubwa ya watumishi wa mkataba katika maeneo yaliyotembelewa;

(e) Ufinyu wa maeneo ya hospitali unaoathiri uendelezaji wa miundombinu hususan ujenzi wa majengo mapya;

(f) Changamoto ya manunuzi ya vifaa tiba na dawa kwa gharama kubwa kuliko uhalisia kwa vifaa tiba na dawa maalum ambazo hazimo kwenye mfumo wa manunuzi wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) hasa kwenye Taasisi/Hospitali zinazotoa huduma za kibingwa na bobezi; na

(g) Changamoto ya ongezeko kubwa la magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kiasi kikubwa unategemea upatikanaji wa fedha. Katika miradi ambayo Kamati imetembelea, kunahitajika jitihada za ziada za kupata fedha ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kuyafikia matarajio ya wananchi ya kupata huduma bora.

### 2.2.2 Utekelezaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati Mwaka 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Wakati Bunge lilipoidhinisha Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa ushauri katika maeneo kumi na mbili (12). Taarifa ya Wizara imeonesha kwamba, kwa kiasi, Serikali imetekeleza ushauri wa Kamati na inaendelea kutekeleza kwa yale ambayo bado hayajatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa ushauri uliotolewa na Kamati ambao bado upo katika hatua ya mchakato wa utekelezaji ni kuhusu Sheria ya Kusimamia Huduma ya Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa Binadamu. Kamati ilishauri Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Muswada wa Sheria hiyo na Taarifa imeonesha kuwa Maandalizi yameanza na kufikia hatua ya ukamilishaji wa andiko la mapendekezo ya kutungwa kwa sheria hiyo. Kamati itaendelea kusisitiza kuwa Serikali iendelee kuzingatia ushauri kwa maeneo yote kama ilivyokuwa imeshauriwa.

### 2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Wizara ya Afya yaliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni **Shilingi 819,977,862,602.14.** Makusanyo haya yanatokana na vyanzo vitatu vya makusanyo ambavyo ni Makao Makuu, Hospitali ya Rufaa za Mikoa na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya. Kielelezo Namba 1, kinaonesha mchanganuo wa kiasi cha fedha zilizokadiriwa kukusanywa na fedha zilizokusanywa kwa kila chanzo hadi mwezi Februari 2026.

**Kielelezo Namba 1: Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli Julai, 2025 hadi Februari, 2026**

| NA | CHANZO CHA MAKUSANYO | KIASI KILICHOIDHINISHWA KUKUSANYWA | KIASI KILICHOKUSANYWA HADI FEBRUARI 2026 | ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Makao Makuu ya Wizara | 74,207,303,307.00 | 45,968,268,378.59 | 62 |
| 2. | Hospitali za Rufaa za Mikoa | 153,792,696,693.00 | 96,421,235,048.31 | 63 |
| 3. | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 591,977,862,602.14 | 352,269,409,839.43 | 59 |
| **JUMLA** | | **819,977,862,602.14** | **494,658,913,266.33** | **60** |

*Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliyowasilishwa kwenye Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imechambua vyanzo vyote vitatu vya makusanyo ya maduhuli ili kubaini maeneo yaliyofanya vizuri na yale ambayo hayakufanya vizuri. Katika chanzo cha makao makuu, uchambuzi umebaini kuwa baraza la radiolojia limeongoza kwa makusanyo ya asilimia 116.94 ikifuatiwa na usajili wa wanafunzi na ada za mitihani asilimia 110.

Aidha, maeneo ambayo hayakufanya vizuri kwenye makusanyo ni pamoja na Baraza la Afya ya Mazingira (25%), Baraza la Optometria (34%) na Baraza la Tiba Asili (45%). Maabara ya Taifa (3%), Elimu ya Afya kwa Umma (9%) na Hospitali ya Kanda Mbeya (43%).

**Mheshimiwa Spika**, Katika chanzo cha Hospitali za Rufaa za Mikoa, imebainika kati ya Hospitali za Rufaa 28, Hospitali za Rufaa za Mikoa tisa (9) zimefanya vizuri kwenye makusanyo kwa kukusanya zaidi ya asilimia sabini (70%) hadi mwezi Februari,

2026. Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro - Mawenzi (86%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro (78%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida (77%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani - Tumbi (85%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma - Maweni (82%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe (79%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita (83%) na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu (76%).

Aidha, Hospitali kumi na tisa (19) hazikufanya vizuri kwenye makusanyo ya maduhuli. Baadhi ya Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songea (39%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara - Ligula (48%) na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara (52%).

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Makusanyo ya Mapato yatokanayo na Utoaji wa Huduma kwa Taasisi, hadi kufika mwezi Februari, 2026 kati ya Taasisi 16, ni Taasisi tatu (3) tu ndiyo zimebainika kufanya vizuri. Taasisi hizo ni Kilimanjaro Christian Medical Centre -KCMC (77%), Hospitali ya Taifa Muhimbili (70%) na Taasisi ya Chakula na Lishe TFNC (84%). Baadhi ya Taasisi ambazo hazijafanya vizuri ni Taasisi ya Saratani Ocean Road (49%) na Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania -CCBRT (41%).

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla hali ya makusanyo ya maduhuli ni ya wastani, kwani inategemewa hadi kumaliza robo ya tatu ya mwaka mwezi Machi, 2026, makusanyo yawe yamefika angalau asilimia sabini (70%). Hivyo ipo haja ya kuhakikisha

makusanyo yote yanapatikana hasa kwa maeneo ambayo hayakufanya vizuri.

### 2.2.4 Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2025/2026


**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Afya (Fungu 52) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,763,541,235,000.00**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 626,433,136,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni **Shilingi 475,418,119,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 151,015,017,000.00.** Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo ziliidhinishwa **Shilingi 1,137,108,099,000.00** ambapo kati yake fedha za ndani ni **Shilingi 789,458,609,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 347,649,490,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Kupitia uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2026 hali ya utolewaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida ni ya kuridhisha kwani fedha zimetolewa kiasi cha **Shilingi 417,383,266,085.48** sawa na **asilimia 67** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa mwaka 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo hali ya upatikanaji wa fedha ni ya wastani kwani kimetolewa kiasi cha **Shilingi 590,628,476,490.18** sawa na **asilimia 59** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilizopokelewa ni **Shilingi 360,535,476,951.31** sawa na **asilimia 46**; na fedha za nje zilizopokelewa ni **Shilingi 230,092,999,538.87** sawa na **asilimia 66**.

Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na fedha zilizotolewa unapatikana katika katika kielelezo Namba 2.

**Kielelezo Namba 2: Fedha zilizoidhinishwa 2025/2026 na Fedha zilizotolewa hadi Februari, 2026**




| | Mshahara | Matumizi Mengineyo | Fedha za Miradi Maendeleo za Ndani | Fedha za Miradi ya Maendeleo Nje |
|---|---|---|---|---|
| Fedha zilizoidhinishwa 2025/2026 | 475,418,119,000.00 | 151,015,017,000.00 | 789,458,609,000.00 | 347,649,490,000.00 |
| Fedha zilizotolewa hadi Februari 2026 | 326,087,395,811.70 | 91,295,870,273.78 | 360,535,476,951.31 | 230,092,999,538.87 |
| Asilimia | 69 | 61 | 46 | 66 |

*Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliyowasilishwa kwenye Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, Imebainika kuwa, miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha za ndani ni miradi hamsini na nane (58). Kati ya miradi hiyo, miradi kumi na saba (17) sawa na asilimia 29 imepokea fedha. Baadhi ya miradi iliyopokea fedha za ndani za maendeleo ni Taasisi ya Saratani Ocean Road, Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko na Kuambukiza, Uimarishaji wa Huduma za Chanjo, Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko, Dawa na Bidhaa za Afya na Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto hospitali ya rufaa ya mkoa wa Songwe.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi arobaini na moja (41) sawa na asilimia 71 haikupokea kiasi chochote cha fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi hiyo. Baadhi ya miradi ambayo haikupewa kiasi chochote licha ya kutengewa fedha za ndani ni pamoja na Udhibiti wa Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza (NCDS), Ujenzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto Dodoma, Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Matibabu ya Magonjwa ya Mlipuko Kagera na Kisopwa *(Isolation Centre)*, Ujenzi wa Hospitali Maalum ya Huduma za Utengamano katika Mkoa wa Tabora, Ujenzi wa huduma za Mama na Mtoto Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga-Bombo, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Burigi, Chato,Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro- Mawenzi, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Morogoro, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, Ujenzi wa jengo la kuifadhia maiti na uzio hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma, Ujenzi wa jengo la OPD na Mama na Mtoto Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi Wing A na B, Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara-Ligula, Ujenzi wa EMD ICU,OPD Utawala na jengo la Mionzi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara, Ujenzi wa OPD Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya,Ujenzi wa jengo la OPD hospitali ya Rufaa ya Arusha-Mount Meru,Ujenzi wa jengo la OPD Complex hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza-Sekou Toure na Ujenzi wa jengo la OPD awamu ya tatu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi-Sokoine.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha za nje za miradi ya maendeleo ziliidhinishwa katika miradi ishirini na moja (21). Kati ya miradi hiyo, miradi kumi na mbili (12) sawa na asilimia 57 imepokea fedha. Baadhi ya miradi hiyo iliyopokea fedha ni mradi wa udhibiti wa magonjwa ya mlipuko na kuambukiza, mradi wa uimarishaji wa huduma za chanjo, mradi wa uimarishaji wa huduma za lishe, mipango ya afya na uendeshaji na mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria.

Aidha, baadhi ya miradi ambayo haikupata fedha za nje zilizoidhinishiwa hadi mwezi Februari 2026 ni program ya maendeleo ya sekta ya afya, mradi wa ujenzi wa hospitali ya mama na mtoto Dodoma, mradi wa ujenzi wa kituo cha umahiri cha matibabu ya magonjwa ya mlipuko Kagera na mradi wa ujenzi wa jengo la mionzi pamoja na ununuzi wa vifaa tiba hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla mwenendo huu wa utoaji fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo si wakuridhisha. Hivyo, ni muhimu sasa, Serikali ihakikishe fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha 2025/2026 kuisha ili kufikia malengo ya utekelezaji wa kila mradi uliokusudiwa.

## 2.3 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ikizingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi huo ulifanyika kwa kujielekeza kwenye maeneo makuu mawili ambayo ni: -

(a) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(b) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa maeneo hayo mahususi unalenga kuhakikisha kuwa makadirio ya mapato yanazingatia uhalisia wa ukusanyaji uliopatikana, na kwamba makadirio ya matumizi yanaendana na uwezo halisi wa upatikanaji wa fedha. Hivyo, kuliwezesha Bunge kupima uhalali, utekelezekaji na ufanisi wa bajeti inayopendekezwa. Kwa msingi huo, uchambuzi huu ndio unaoliwezesha Bunge kufanya uamuzi sahihi na wenye kuzingatia nidhamu ya fedha za umma.

### 2.3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni **Shilingi 747,200,091,299.81.** Kielelezo Namba 3 kinaonesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo kutoka katika kila chanzo.

**Kielelezo Na: 2 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Fungu 52 kwa Mwaka 2026/2027**

| CHANZO CHA MAKUSANYO | KIASI |
|---|---|
| Makao Makuu ya Wizara | 76,195,850,735.53 |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa | 165,804,149,264.47 |
| Taasisi, Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda | 505,200,091,299.81 |
| **JUMLA** | **747,200,091,299.81** |

*Chanzo: Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2026/2027 iliyowasilishwa kwenye Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umebainisha kupungua kwa kiasi cha makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2026/2027. Kiasi kilichopungua ni **Shilingi 72,777,771,302.33** sawa na upungufu wa asilimia tisa **(9%)** ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichokadiriwa kukusanywa mwaka 2025/2026. Upungufu huu upo katika chanzo cha makusanyo ya Taasisi ambapo baadhi ya Taasisi zimekadiriwa kukusanya kiasi kidogo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026. Baadhi ya Taasisi zilizopunguziwa makadirio ya makusanyo ni pamoja na Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasi, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa

Magonjwa ya Binadamu-NIMR na Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania-CCBRT.

**Mheshimiwa Spika**, Kielelezo Namba 4, kinaonesha mchanganuo wa ulinganisho wa fedha za makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2025/2026 na 2026/2027.

**Kielelezo namba 3: Ulinganisho wa Fedha za Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027**

| **Maelezo** | **Makadirio ya Makusanyo 2025/2026** | **Makadirio ya Makusanyo 2026/2027** | **Kiasi Ongezeko** | **Ongezeko au Pungufu (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Makao Makuu | 74,207,303,307.00 | 76,195,850,735.53 | 1,988,547,428.53 | **+3** |
| Hosp za Rufaa za Mikoa | 153,792,696,693.00 | 165,804,149,264.47 | 12,011,452,571.47 | **+8** |
| Taasisi | 591,977,862,602.14 | 505,200,091,299.81 | 86,777,771,302.33 | **-15** |
| **JUMLA KUU** | **819,977,862,602.14** | **747,200,091,299.81** | **72,777,771,302.33** | **-9** |

***Chanzo;*** *Randama ya Wizara ya Afya 2026/2027 iliyowasilishwa kwenye Kamati*


**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi unaonesha makadirio ya makusanyo kutoka vyanzo vya makao makuu ya Wizara na hospitali za rufaa za Mikoa yameongezeka wakati chanzo cha makusanyo kutoka katika Taasisi yamepungua. Hata hivyo, ili kuhakikisha makusanyo yanayokadiriwa yanapatikana kwa uhakika, ni vema Serikali kuhakikisha inakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuzuia uvujaji wa mapato.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2026/2027 Wizara ya Afya imetengewa **Shilingi 1,800,262,058,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 652,236,871,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 135,913,515,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 516,323,356,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi.

**Mheshimiwa Spika**, Fedha zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni **Shilingi 1,148,025,187,000.00**. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni **Shilingi 789,458,609,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 358,566,578,000.00.** Kielelezo Namba 5 kinaonesha mchanganuo wa fedha zinazoombwa kuidhinishwa.

**Kielelezo namba 5: Mchanganuo wa Fedha zinazoombwa Kuidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**




***Chanz:;** Randama ya Wizara ya Afya 2026/2027 iliyowasilishwa kwenye Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Imebainika kuwa fedha zinazoombwa kuidhinishwa mwaka 2026/2027 kwa ajili ya Wizara ya Afya (Fungu 52) zimeongezeka kwa **Shilingi 36,720,823,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 2** ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa mwaka 2025/2026. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Afya mwaka hadi mwaka. Aidha, ongezeko hili la **asilimia 2** ya fedha zinazoombwa kwa mwaka 2026/2027 lipo katika fedha za mishahara ambazo zimeongezeka kwa **asilimia 9** na fedha za nje za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 3**.

**Mheshimiwa Spika**, Kielelezo Namba 6 kinaonesha mchanganuo wa ongezeko la fedha kwa ulinganisho wa bajeti ya mwaka 2025/2026 na 2026/2027.

**Kielelezo namba 6: Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa Mwaka 2025/2026 na Fedha zinazoombwa kuidhinishwa Mwaka 2026/2027**

| MAELEZO | 2025/2026 (Shilingi) | 2026/2027 (Shilingi) | Ongezeko/ Pungufu | Ongezeko/ Pungufu |
|---|---|---|---|---|
| Mishahara | 475,418,119,000.00 | 516,323,356,000.00 | +40,905,237,000.00 | +9% |
| Matumizi Mengineyo | 151,015,017,000.00 | 135,913,515,000.00 | -15,101,502,000.00 | -10% |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA** | **626,433,136,000.00** | **652,236,871,000.00** | **+25, 803, 735,000.00** | **+48%** |
| Fedha Maendeleo (Ndani) | 789,458,609,000.00 | 789,458,609,000.00 | 0 | 0% |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 347,649,490,000.00 | 358,566,578,000.00 | +10,917,088,000.00 | +3% |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA MIRADI YA MAENDELEO** | **1,137,108,099,000.00** | **1,148,025,187,000.00** | **+10,917,088,000.00** | **+1%** |
| **JUMLA KUU YA BAJETI** | **1,763,541,235,000.00** | **1,800,262,058,000.00** | **+36,720,823,000.00** | **+2%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Wizara ya Afya 2026/2027 iliyowasilishwa kwenye Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Ni imani ya Kamati kuwa, Serikali itaendelea kuongeza fedha kwa ajili ya Wizara ya Afya ili kuongeza kasi ya kuboresha sekta hii muhimu inayogusa maisha ya kila Mtanzania. Aidha, ni muhimu kwa fedha zote zinazoidhinishwa kutolewa kwa wakati ili kutimiza malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha husika.

## 2.4 Masuala Mengine Muhimu kuhusu Mpango wa Wizara kwa Mwaka wa fedha 2026/2027

### 2.4.1 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

**Mheshimiwa Spika,** Katika taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati mwezi Machi, 2026, Kamati imejulishwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ili kuinusuru MSD ikiwa ni pamoja na kujenga maghala makubwa mawili yaliyogharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 42.3** katika Mkoa wa Dodoma na Mtwara. Vilevile, kupunguza deni la bidhaa za miradi misonge kwa kulipa kiasi cha **Shilingi bilioni 50**.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto ambazo zimekuwa zinaikabili Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ni ukosefu wa mtaji na madeni inayoidai Serikali. Madeni hayo yamegawanyika katika makundi mawili na yamekuwa yakiongezeka kila mwaka. Kundi la kwanza ni bidhaa zinazotolewa kwa vituo vya kutolea

huduma za afya nchini kwa matarajio ya kulipwa pindi vituo vitakapokuwa na fedha. Kundi la pili ni gharama za Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Miradi Misonge ambapo Serikali iliingia makubaliano ya kuchangia gharama. Jumla ya madeni yote ni takribani **Shilingi bilioni 302.2.**

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa madeni ya bidhaa zilizosambazwa unaonesha kuwa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyopo chini ya Wizara ya Afya vinadaiwa **Shilingi bilioni 46.4** na vituo vilivyopo chini ya OWM-TAMISEMI vinadaiwa **Shilingi bilioni 83.1**. Kwa upande wa bidhaa za afya za miradi misonge, Serikali inadaiwa **Shilingi bilioni 172.7.**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa changamoto ya mtaji katika mwaka wa fedha 2022/2023, ombi la kupewa mtaji liliwasilishwa kupitia Wizara ya Afya. Lengo la mtaji huo unaoombwa ni kuongeza ufanisi wa Bohari Kuu ya Dawa ili itekeleze vema majukumu yake ambayo ni Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Afya.

**Mheshimiwa Spika**, Mtaji unaoombwa ni **Shilingi bilioni 300** kwa mchanganuo wa **Shilingi bilioni 150** kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa dawa, **Shilingi bilioni 110** kwa ajili ya kulipa madeni ya washitiri, **Shilingi bilioni 24.1** kwa ajili ya ujenzi wa Maghala, **Shilingi bilioni 15.4** kwa ajili ya ujenzi wa Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Ni vema Serikali ikaipa kipaumbele MSD kwa kuipa mtaji kwani, ikiwa kiasi kinachoombwa cha mtaji kitapatikana kitaiwezesha Bohari Kuu ya Dawa kununua mahitaji yote ya bidhaa za Afya bila kusubiri fedha za vituo vya

kutolea huduma za Afya. Aidha, madeni yote Serikali inayodaiwa yatafutiwe ufumbuzi ili kunusuru ustahimlivu wa Bohari Kuu ya Dawa.

### 2.4.2 Uwekezaji wa Viwanda vya Kuzalisha Bidhaa za Afya

**Mheshimiwa Spika**, Uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya nchini ni eneo la kimkakati linalolenga kuimarisha sekta ya afya, kutoa ajira, kupunguza utegemezi wa uagizaji wa dawa kutoka nje, na kukuza uchumi wa viwanda pamoja na kuiweka Tanzania kwenye ramani ya uzalishaji wa bidhaa za afya barani Afrika na duniani. Hii ni azma ya Serikali kama ilivyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2025 – 2030, kwamba kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji/sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata mwaliko wa kushiriki katika Mkutano wa tarehe 19 Januari 2026 ambapo Waziri wa Afya aliitisha Mkutano mkubwa wa wawekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba lengo likiwa ni kuifanya Tanzania kuongeza uzalishaji kufikia zaidi ya asilimia sitini (60%) na kuwa kitovu cha uzalishaji kikanda ifikapo 2030.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani wa viwanda vya dawa, Ni vema kuhakikisha kunakuwepo mazingira rafiki na wezeshi ambayo yatavutia uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuondoa urasimu, kutoa vivutio vya kodi na kuboresha miundombinu.

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati ina maoni kuwa, hatua kubwa iliyofikiwa katika maboresho ya huduma za afya nchini, inatokana na dhamira ya kweli ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujali afya kwa watu wake. Serikali inastahili pongezi kwa juhudi kubwa ya kuboresha huduma za afya nchini. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa huduma za afya na kuiboresha Sekta hii muhimu kwa Taifa kwa kufanya mambo mbalimbali kama : -

(i) Kuanza awamu ya kwanza ya majaribio ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote;

(ii) Kuwa na maono ya Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili *(New Muhimbili)*;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya Hospitali za Rufaa za Mikoa; na

(iv) Kununua vifaa tiba vya kisasa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa. Mfano ununuzi wa mashine ya PET CT SCAN, MRI (Magnetic Resonance Imaging), Angio Suite, Mammography na Hyperbaric Chamber.

### 3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na maoni hayo kuhusu azma ya Serikali, ushauri unaotolewa na Kamati unachochewa na miongozo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (2050), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa

Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka Mmoja (2026/27), Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025 - 2030, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya (HSSP-V 2021-2026), Mpango Mkakati wa Wizara 2020/2021-2025/2026 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's 2030).

Kwa msingi huo, Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

**(a) Upungufu wa Rasilimali Watu**

Kutokana na upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya hususan kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vinavyosimamiwa na Wizara ya Afya, Serikali -

(i) Iendelee kutoa vibali vya ajira kwa kada zinazokabiliwa na upungufu katika vituo vya kutolea huduma za afya;

(ii) Iendelee kutoa ufadhili wa masomo kwa wataalam wa afya ili kupata mafunzo ikiwemo mafunzo ya huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi; na

(iii) Vibali vya ajira vitolewe kwa kuzingatia ikama ya Taasisi husika na kipaumbele kiwe kwa wataalam wanaojitolea kutoa huduma za afya katika hospitali mbalimbali nchini.

**(b) Mwenendo Usioridhisha wa Utolewaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo**

Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa mwaka 2025/2026 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili miradi iliyokusudiwa ikamilike mapema na kuwanufaisha wananchi.

**(c) Mwenendo hafifu wa Makusanyo ya Maduhuli**

Serikali iendelee kuzijengea uwezo Taasisi zake katika mifumo, utoaji wa huduma bora na ukusanyaji wa maduhuli ili kuwepo na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wote.

**(d) Kasi ndogo ya Ukamilishaji wa Miradi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa**

Serikali iweke kipaumbele cha kutoa fedha katika miradi ambayo imeanza muda mrefu ili ikamilike na kuanza kutoa huduma. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya hospitali nchini uende sambamba na ununuzi wa vifaa tiba ili kuleta tija kwa jamii.

**(e) Ukosefu wa Mtaji Bohari Kuu ya Dawa (MSD)**

Serikali itoe mtaji wa **Shilingi bilioni 300** kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ili kuongeza ufanisi na kuboresha upatikanaji wa bidhaa za Afya, kusaidia uwekezaji kwenye viwanda na kuongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa za afya kwa kujenga maghala ya kutosha. Kukosekana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.

**(f) Madeni ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa Serikali**

Serikali ilipe deni linalodaiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) lenye thamani ya **Shilingi bilioni 302.2**, kwa mchanganuo wa **Shilingi bilioni 46.4** kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyopo chini ya Wizara ya afya, Shilingi **bilioni 83.1** kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyopo chini ya OWM-TAMISEMI na **Shilingi bilioni 172.7** za miradi Misonge. Ni muhimu sana madeni haya yakalipwa ili kuendelea kuulinda mnyororo wa ugavi na kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa wakati na kwa utoshelevu.

**(g) Uimarishaji wa Viwanda vya Ndani vya Kuzalisha Bidhaa za Afya**

Serikali iendelee kuweka mazingira wezeshi na rafiki yatakayovutia wawekezaji wengi wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya nchini.

**(h) Uimarishaji wa Huduma za Kinga**

Serikali iimarishe huduma za kinga kwa kuwekeza zaidi kwenye kinga kwani ndio msingi muhimu wa afya. Ikiwa huduma za kinga zitaimarishwa zaidi, zitasaidia sana hupunguza gharama za matibabu na kuokoa maisha hivyo kuwa na jamii yenye afya bora na yenye nguvu kazi ya kutosha kwa maendeleo ya Taifa.

## 3.3 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, Afya ni msingi wa Taifa lolote Duniani unaobeba Sekta zote nchini. Hakuna maendeleo ya kweli bila uwekezaji wa kutosha katika huduma za afya. Hivyo, Serikali ina wajibu wa kuendelea kuimarisha huduma za afya kwa kuwekeza kwa kununua mitambo ya matibabu na kuongeza huduma za kibingwa ikiwa ni kichocheo cha maendeleo ya Uchumi na Ustawi wa Jamii.

## 3.4 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Aidha, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee nawashukuru sana Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mb)-Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi (Mb)-Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Abdallah Shekalage, Naibu Katibu Mkuu Ndugu. Ismail Rumatila pamoja na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulika na masula ya dawa na vifaa tiba Ndugu. Emmanuel Tayari. Vilevile, namshukuru Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Elias Magembe pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote inapotekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee nawashukuru sana wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe hawa wameshiriki kikamilifu katika kujadili na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Johannes Lembulung Lukumay, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, Mb – **M/MWENYEKITI**
3. Mhe. Jacqueline Kainja Andrew, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Adonis Alfred Bitegeko, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Janeth Peter Pinda, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Juma Mustafa Kawamba, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Japhael Masanja Lufungija, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Husnain Gulamabbas Dewji, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Muhsin Haji Ussi, Mb -Mjumbe
14. Mhe. Nadra Ghulam Rashid, Mb -Mjumbe
15. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb -Mjumbe
16. Mhe. Eric James Shigongo, Mb -Mjumbe
17. Mhe. Yagi Maulid Kiaratu, Mb -Mjumbe
18. Mhe. Jamila Mahmoud Juma, Mb -Mjumbe
19. Mhe. Neema William Mgaya, Mb -Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu. Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema na kwa wakati wote.

**Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyoombwa na mtoa hoja.**

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Johannes L. Lukumay (Mb),
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**
11 Mei, 2025